

Utoaji Mimba Na Dr. George Tiller

Mnamo Mei 31, 2009 Dr. George Tiller alipokuwa akipitisha vijarida pale Evangelical Lutheran Church (ELCA) aliuawa. Kwa mara ya kwanza nilipata habari hii, hisia nyingi zilizochanganyikana ziliingia akilini mwangu. “Jicho kwa jicho, jino kwa jino,” Kutoka 21:24. “Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu,” Mwanzo 9:6. “wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, kisasi ni juu yangu mimi nitalipa, anena Bwana,” Warumi 12:19. “Waambie, kama niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwa mtu mwovu; bali aghairi mtua mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, enyi nyumba ya Israel? Ingawaje nimechanganya hisia juu ya mtu huyu, Yesu alikufa kwa ajili yake pia, Yohana 3:16. Na endapo angelitubu (2 Petro 3:9) na akabatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Matendo ya mitume 2:38), naye angaliokolewa (Matendo ya mitume 2:40-41). Lakini nijualo kwa hakika kuhusiana na Dr. George Tiller ni kwamba sasa yuko katika mateso akiomba mtu aende nyumbani kwake kushuhudia kuhusiana na Bwana wetu Yesu Kristo, Luka 16:27-28, Pili, anataka huyo mtu aende athibitisha kwamba utoaji mimba ni uuaji, na wauaji wote watatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, Ufunuo 21:8.

Sikumbuki ni watoto wangapi ambao Dr. George Tiller aliwaua. Lakini alikuwa mashuhuri kwa kuwa mmoja wa wauaji wa mwisho mwisho, na nimesikia madai kwamba aliua hadi watoto wapatao 60,000 mwishoni. 60,000, ambayo ni miji 3,000 yenye ukubwa kama Kountze, Texas waliouliwa na mtu huyu peke yake. Sasa, hebu tuone Biblia inasemaje kuhusiana na watoto wawapo tumboni, mauaji na wanachoamini leo Walutheri kuhusiana na utoaji mimba.

Biblia inathibitisha waziwazi kwamba kutoa mimba ni mauaji na ni dhambi. Tazama aya hizi (nazo ni chache tu kati ya nyingi ambazo zingeorodheshwa):

Yakobo 2:26 – “Mwili pasipo roho umekufa.” La muhimu hapa ni kuwa, kama kuna mwili, na mwili uko hai, basi kuna roho iliyounganika nao.

Kumbukumbu la Torati 12:23 – “Damu ndiyo uhai.” Mtoto anapata mfumo wake wa damu akiwa tumboni baada ya juma la nne tangu kutungwa mimba.

Mwanzo 5:3, 4, 28-30, n.k. “akamzaa mwana.” Amkazaa, huelezea kutunga mimba na urutubishaji wa yai, na zingatia baada ya kutunga ndipo hutajwa kwamba wazazi wakamzaa mwana. Yakobo 3:23; 4:17; 10:5; panaweza kusaidia

kufafanua hili. Ayubu alipokuwa tumboni mwa mamaye tayari alikuwa “mtoto mume” Ayubu 3:2-3; 4:17; 10:5.

Mwanzo 25:21-22 – Twasoma habari ya Rebeka akiwa na mimba ya mapacha, na tazama! wale mapacha, Mungu anawaita “watoto” ili hali bado wako tumboni.

Hivyo, hebu na tuone aya zifuatazo vile vile;

Mwanzo 4:10 Baada ya Kaini kumuua Habili, damu ya Habili ilikuwa inalia kutoka ardhini

Zaburi 5:6 – “Bwana humzira muuaji na mwenye hila.”

Kumbukumbu la Torati 27:25 – “Na alaaniwe atwaaye ujira wa kumuua asiye makosa.”

Mithali 24:11-12 – “Je, hatamlipa kila mtu sawa sawa na kazi yake.”

Jambo lingine lililonigutusha mara niliposikia mauaji haya ya Dr. Tiller ni pale ni lile jambo kwamba alikuwa akipitisha vipeperushi katika mkusanyiko wa ibaada ya “kikristo”. Naelewa kwamba wengine watakuwa hawakujua kweli ya Neno la Mungu kama ukweli huo uliwapita. Lakini kumkaribisha mtu anayejulikana kuwa mtoa mimba nafikiri ni jambo ambalo hakuna anayekiri kuwa mtauwa angelifanya. Sasa sisemi na wala sidai kwamba Kanisa la Kilutheri ni Kanisa ambalo Kristo alilijenga, Mathayo 16:18. Lakini wanadai kwamba wao ni Kanisa lile ambalo Kristo alilijenga. Basi haiwapasi kuyatii maneno ya Muumba? Yohana 14:16.

Dr. Tiller alikuwa ni muumini wa Kanisa la Kilutheri kigango cha Missouri. Walakini, siku kadhaa nyuma alikaripiwa kutokana na dhambi zake, naye aligoma kutubu na wakamtenga. Ndipo basi akaenda kujiunga na Evangelical Lutheran Church in America, dhehebu ambalo ni kubwa sana Marekani. Kwa mujibu wa katiba yao Kanisa la Kilutheri iliyoidhinishwa mwaka 1991, wanadai kwamba lengo lao ni kutetea uhai isipokuwa katika vipengele vitatu (1- Uhai wa mama unapokuwa hatarini; 2-ujauzito umetoka 3- Mimba imetokana na maingiliano baina ya watu ambao ni ndugu wa damu.) Walieleza vile vile kwamba kijusi (kiumbe mwenye umri wa wiki nane kabla ya miezi tisa tangu yai kurutubishwa) ataweza kuishi nje ya tumbo la mama kwa msaada wa kiteknolojia. (Utoaji mimba wa kisasa)? Kwa jinsi gani?

Ndugu katika Bwana, hii ndiyo sababu tunatakiwa kujihadhari na mafundisho potofu, 1 Timotheo 4:1, kwa sababu hutushawishi tuikubali dhambi kana kwamba si kitu. Na mara mtu au kikundi cha watu kianzapo kuelekea katika poromoko hilo, huishia wapi? Kwa upande wa ELCA, mwisho wake unathibitisha kwamba watajari kidogo ukweli uliopo katika Biblia. Wakati wa kongamano la Agosti 17-23, 2009 ELCA walikutana ili kuendeleza “hoja ya kiraia iliyokuwa imependekezwa juu ya unyumba.” Hata sielewi ilihusu nini?